**MULIKA Na. 40(2) 2021 (109-123)**

# Dhima ya Sadfa ya Kimapenzi katika Kujenga Matukio ya 'Kishushushu' na 'Kijasusi': Uchunguzi wa Riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*

*Gervas A. Kasiga*[1]
Chuo Kikuu cha Dodoma

*na*

*Eliamini M. Maffa*[2]
Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dodoma

## Ikisiri

Shabaha ya makala haya ni kufafanua matumizi ya sadfa ya kimapenzi katika kuwasaidia watunzi kujenga tungo mbalimbali za kisanaa na kutimiza au kukamilisha uwasilishaji wa matukio ya kishushushu na kijasusi. Ufafanuzi wetu umemakinikia riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* ya mwandishi Aristablus Elvis Musiba. Sadfa ni hali ya utokeaji wa matukio kwa wakati mmoja kwa namna inayoshangaza au inayoashiria bahati. Hii ni miongoni mwa mbinu zinazotumiwa na watunzi katika kuzijenga na kuzikamilisha tungo zao (Wamitila, 2003; Dannenberg, 2008). Mara nyingi watunzi wa kazi za kifasihi huitumia mbinu hii sambamba na mbinu nyingine katika kufanikisha azma ya tungo hizo. Mbinu hizo nyingine zaweza kuhusisha uhalisiajabu, utanzia, ufutuhi, na usemezano. Kazi ya kifahisi hujengwa kwa kutumia mbinu mbalimbali za kisanaa zinazoafikiana na lengo pamoja na aina ya kazi ya kifasihi inayowasilishwa. Sadfa ni mojawapo ya mbinu hizo za kisanaa ambayo hutumiwa na watunzi kuibua, kujenga na kukamilisha azma ya tungo zao. Katika mjadala wa makala haya tumeonesha namna sadfa ya kimapenzi ilivyotumika kwenye miktadha ya kutiana moyo wa kufanikisha kazi ya kishushushu na kijasusi; kuleta urahisi wa ufanikishwaji wa kazi ya kishushushu na kijasusi; kusaidia uokozi na uchocheaji kisasi; na mwishowe kusababisha uvumbuzi wa taarifa muhimu za kijasusi pamoja na ukamilishwaji wa operesheni za kijasusi. Katika riwaya teule mwandishi ameitumia mbinu hii kupitia mahusiano ya kimapenzi baina ya mhusika wake mkuu Willy Gamba (mwanamume) pamoja na wahusika wasaidizi (mabinti) Amanda, Ntumba, Mwadi na Tete.

## 1.0 Utangulizi

Kama ilivyobainishwa awali, sadfa ni mbinu muhimu katika msuko wa matukio yajengayo tanzu mbalimbali za fasihi. Umuhimu wake kwa kiasi kikubwa, hutokana na nafasi yake ya kuibua taharuki na kuchangamsha wasomaji wa

[1] **Barua pepe**: *kassiga@gmail.com*
[2] **Barua pepe:** *eliaminmark@gmail.com*

masimulizi husika (Wamitila, 2002). Sadfa huweza kugawanywa kulingana na miktadha ya utumikaji wake. Mathalani, sadfa huweza kujiibua kupitia hali ya ukamilishanaji wa matukio ya kimasimulizi, kipelelezi, na katika mahusiano ya kimapenzi baina ya wahusika waliojengwa katika kazi ya kifasihi.

Kimsingi, sadfa zilizo katika mfumo wa kipelelezi huambatana na mchakato mzima wa kuchunguza, kutafiti, kugundua na kuchukua hatua (Wafula na Njogu, 2007). Aina hii ya sadfa huweza kuchukuana pamoja na matukio mengine ya kihalifu au/na kimapenzi baina ya wahusika. Sadfa za ukamilishaji wa matukio zenyewe hujengwa kwa minajili ya kuchagiza kukamilika kwa matukio ya masimulizi. Kwa hali hiyo, mfumo mzima wa masimulizi hukamilika kwa kutawaliwa na sadfa. Matukio hayo hufikia mwisho baada ya mapambano ya muda mrefu kati ya wahusika kinzani (Kyando, 2012).

Aina nyingine ya sadfa ni ile inayojiibua kupitia mahusiano na mapenzi baina ya wahusika. Hii hutambulika kama sadfa ya kimapenzi. Hutambulika hivi kwa sababu mapenzi huanzishwa kwa sadfa, na kisha kuja kuzalisha matokeo yanayojipambanua kadiri ya mwendelezo wa masimulizi. Ujitokezaji wa matokeo hayo ambayo aghalabu huwa chanya kwa mhusika mkuu, hudhihirisha kuwa ni sadfa tu ndiyo imesaidia kufanikisha tukio lililojengwa (Dannenberg, 2008; Wamitila, 2003). Kupitia makala haya imebainika kuwa sadfa za kimapenzi aghalabu zimekuwa zikijipambanua kupitia riwaya pendwa hususani za kishushushu au kijasusi (Wafula na Njogu, 2007). Kadhalika, ilithibitika kuwa lengo la kutumika kwake katika kazi hizo ni kukamilisha au/na kufanikisha hatua mbalimbali za kiupelelezi, na kuipeleka simulizi kwenye hitimisho.

Katika makala haya aina hiyo ya sadfa ndiyo msingi wetu wa kuendeshea mjadala. Makala yanalenga kujadili dhima ya mbinu ya sadfa ya kimapenzi katika kufanikisha ujenzi wa matukio ya kishushushu na kijasusi. Mdhihiriko wa matumizi yake umebainishwa kupitia hali iliyotawaliwa na mahusiano, pamoja na mapenzi baina ya wahusika wa jinsi tofauti kupitia riwaya teule ya *Kikosi cha Kisasi.* Matumizi maalumu ya mbinu ya sadfa ya kimapenzi katika riwaya hiyo yamemakinikiwa kupitia mahusiano kati ya Willy Gamba (mwanamume) na mabinti Amanda, Ntumba, Mwadi na Tete.

Aidha, makala haya yamechagua kushughulikia riwaya ya kipelelezi kwa sababu zifuatazo: mosi, asili ya matukio yajengayo masimulizi yaliyoshughulikiwa yametawaliwa na matukio yenye ushushushu na ujasusi; pili, ukamilishwaji wa matukio umepewa hamasa zaidi na kuwapo kwa matukio ya kimapenzi ndani yake; tatu na mwisho, ni kubainika kutumika kwa sadfa ya kimapenzi katika kufanikisha harakati zote za ushushushu na ujasusi katika masimulizi ya riwaya teule. Hivyo, basi, riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* imekuwa chaguo letu kutokana na kuwapo kwa matukio mengi yenye mwelekeo unaoendana na mada ya makala haya.

**1.1 Dhana za Upelelezi, Ushushushu na Ujasusi**

Upepelezi ni dhana inayoelezea uchunguzi maalumu wa kiintelijensia kwa ajili ya kuilinda nchi dhidi ya viashiria vinavyohatarisha usalama wake (Chahali, 2016). Mchakato wa jambo hili kwa nchi husika hufanyika kupitia viapo maalumu na sheria. Viapo hivi na sheria humsaidia mtekelezaji wa shughuli za upelelezi kuweza kukusanya taarifa na ushahidi wenye ukweli kuhusu uhalifu unaotarajiwa kutendeka au/na uliotendeka. Katika hatua za upelelezi taarifa hukusanywa, huchambuliwa na kutolewa mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa. Wakati mwingine hatua hizo huenda sambamba na matumizi ya nguvu za kimapambano ili kuweza kuzifanikisha. Shughuli za upelelezi huongozwa na afisa upelelezi/afisa usalama wa taifa. Afisa upelelezi hufanya kazi ya kupeleleza watu kwa niaba ya serikali na kwa manufaa ya taifa lake (TUKI, 2013). Afisa huyu anapofanya kazi katika nchi ya uraia wake huitwa shushushu. Hata hivyo, afisa anapofanya kazi nje ya taifa lake hufanya shughuli ya kijasusi. Hii ni kwa sababu hudukua siri za nchi jirani au za mbali kwa manufaa ya nchi yake ya asili (Chahali, 2016).

Upelelezi ni kazi inayohitaji ujasiri mkubwa. Katika hali halisi, shughuli za kipelelezi zimekuwa zikiyagharimu maisha ya wapelelezi ulimwenguni. Mathalani, hivi karibuni katika matukio halisi mpepelezi wa Shirika la Ujasusi la Kimitandao la Kimarekani (NSA), Edward Snowden, aliikimbia nchi yake ya Marekani na kwenda kuishi uhamishoni (Urusi) kutokana na kukiuka miiko ya kazi yake (Snowden, 2019). Miiko ya kazi ya upelelezi inapovunjwa, ni kawaida kwa afisa anayehusika kuadhibiwa kifo. Hivyo, Bwana Snowden alieleza siri za shirika lake hadharani kwa kufafanua jinsi shirika hilo la kijasusi linavyodukua taarifa za watu katika mitandao. Jambo hilo limesababisha atafutwe kwa udi na uvumba na vyombo vya usalama vya Marekani ili akayajibu mashtaka ya uhaini dhidi ya nchi yake ya Marekani.

Pia, nchini Tanzania, Evarist Chahali aliyekuwa Afisa Usalama wa Taifa aliamua kutorokea Uskochi nchini Uingereza kukwepa tuhuma dhidi yake za kwenda kinyume na kiapo cha kazi yake na nchi yake (Chahali, 2016). Kuna mifano anuwai inayoonesha kuwa ushushushu na ujasusi ni kazi nyeti na ya hatari inayohitaji moyo wa ujasiri na kujitoa. Katika simulizi ya kweli ya "Mateka Mpakani" napo yanaelezwa masaibu aliyoyapata aliyekuwa Afisa Usalama wa Jeshi la Wananchi la Tanzania (JWTZ), Meja wa Jeshi Mstaafu, Frowin Kageuka, na wenzake watatu ambao waliwekwa mtegoni na kisha kukamatwa na majeshi ya Uganda. Maafisa usalama hao wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania walikuwa wakifanya shughuli za ujasusi dhidi ya majeshi ya Nduli Iddi Amini Dada (Kageuka, 2016). Hii yote ni mifano inayozidi kuonesha ugumu wa kazi hii.

Vilevile, masimulizi ya Mzee Peter D. M. Bwimbo yanathibitisha namna kazi ya uafisa usalama ilivyo hatari (Bwimbo, 2015). Mzee huyu alikuwa mlinzi mkuu wa Rais Julius Kambarage Nyerere. Katika masimulizi yake anaeleza namna alivyojitoa mhanga kumtorosha Rais Nyerere wakati wa uasi wa jeshi la iliyokuwa serikali ya Tanganyika. Kwa muhtasari, kazi ya upelelezi ni ya kufa au kupona.

Mafunzo yake huhitaji uwezo mkubwa wa utumiaji akili inayoenda sambamba na mafunzo maalumu ya kutumia mbinu za mapambano ya mwili na utumiaji wa silaha za kawaida na moto.

Kwa sababu kazi za kifasihi husawiri maisha ya kijamii, masuala ya kipelelezi, kishushushu, na kijasusi nayo yamekuwa yakijichomoza katika kazi hizo. Katika ujenzi wa riwaya za kipelelezi za Kiswahili mambo hayo yamekuwa yakijichomoza kupitia masimulizi yanayotawaliwa na matukio yenye ufundi wa kiuchunguzi na mapigano baina ya pande mbili zinazokinzana (Madumulla, 2009). Kwa kiwango kikubwa mambo hayo yamebainika katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* tuliyoiteua kufanyia mjadala wetu. Katika riwaya hiyo, Willy Gamba ambaye ni mhusika mkuu amebebeshwa sifa bainifu za uafisa upelelezi/usalama anazozitumia kufanya ushushushu na ujasusi. Kupitia ufundi wa kisanaa wa mwandishi anatumia sifa hizo kwa kuzinogesha na utumiaji wa sadfa ya kimapenzi katika kuyakamilisha majukumu ya Willy Gamba.

**1.2 Muhtsari wa Riwaya ya Kikosi cha Kisasi**

Riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* imejihusisha na usimuliaji wa operesheni ya kukomesha mauaji ya mfululizo yanayofanywa dhidi ya wapigania uhuru wa Afrika. Mauaji hayo yalichagiza kukwama kwa harakati za kutafuta uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika. Riwaya hiyo inaonesha juhudi mbalimbali zinazofanywa na vyombo vya ulinzi vya nchi huru za Kiafrika ili kutafuta chanzo cha mauaji zinashindwa kuzaa matunda. Ndipo Kamati ya Ulinzi ya Ukombozi wa Umoja wa Afrika inaamua kumpa kazi mpelelezi maarufu Willy Gamba awaongoze wapelelezi wenzake mashuhuri wa Afrika katika kutafiti na kutokomeza mauaji hayo. Willy Gamba (mhusika mkuu wa riwaya hii) ni mpelelezi aliyejizolea sifa kemkem katika maeneo mbalimbali ya Afrika na ulimwenguni kote kwa njia anazotumia kubaini vyanzo mbalimbali vya matatizo.

Kikosi hiki kinawajumuisha Willy Gamba na wapelelezi wengine maarufu wa Afrika (Robert, Ozu na Kofi). Kikosi kinaingia Kinshasa (mji mkuu wa iliyokuwa Zaire, hivi sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo) kwa siri ili kubaini chanzo cha mauaji hayo na wahusika wa mauaji. Taarifa za kuingia kwao Kinshasa zinavuja na zinawapa wakati mgumu zaidi katika kutekeleza mipango yao. Umahiri wao wa kipelelezi na kijasusi unawasaidia kuwapata washirika na wahusika wa mauaji hayo. Mapigano baina ya pande hizo yanasababisha jiji la Kinshasa kuwaka moto. Mbinu za hali ya juu katika mapigano zinakisaidia Kikosi cha Kisasi kushinda vita hiyo.

**2.0 Uchambuzi wa Dhima ya Sadfa ya Kimapenzi katika Riwaya Teule**

Kwenye sehemu hii tumejadili matumizi ya sadfa ya kimapenzi katika kujenga matukio ya kishushushu na kijasusi kama inavyodhihirishwa katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*. Uchambuzi wetu umebainisha kuwa sadfa ya kimapenzi ni muhimu katika ujenzi na ukamilishaji wa matukio ya namna hiyo. Imethibitika kuwa sadfa hii ilijikita katika kutoa moyo kwa mhusika mkuu (Willy Gamba) ili

aweze kufanikisha operesheni ya kishushushu na kijasusi; kuleta urahisi katika hatua za ufanikishaji wa kazi ya kishushushu na kijasusi; kusaidia uokozi na uchocheaji kisasi; na mwisho kufanikisha uvumbuzi wa taarifa muhimu za kishushushu. Katika riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*, sadfa ilidhihirika kupitia ujenzi wa matukio ya kimahusiano baina ya Willy Gamba, Amanda, Ntumba, Mwadi, na Tete.

### 2.1 Sadfa ya Kimapenzi Huwatia Moyo Wahusika

Sadfa hii imejengwa katika muktadha wa kitangulizi cha shughuli za kishushushu na kijasusi kwa mantiki ya kutiana moyo. Aina hii ya sadfa inajiibua pindi Willy Gamba anapokutana na Amanda ambaye ni mfanyakazi wa Idara ya Upepelezi ya Zambia. Idara hiyo ya upelelezi nchini Zambia ilikabidhiwa jukumu la kufanikisha safari ya Willy Gamba ya kwenda nchini Zaire kwa ajili ya kazi maalumu ya kijasusi. Ilibainika kuwa mwandishi aliyajenga makutano yaliyozaa mahusiano baina ya Willy Gamba na Amanda kwa minajili ya kumtia moyo wa kijasiri Willy Gamba katika kufanikisha kazi ya kijasusi aliyopangiwa akaitekeleze nchini Zaire.

Mbinu hii inajipambanua kupitia makutano baina ya Amanda na Willy Gamba katika ofisi hiyo ya kipepelezi. Mwandishi anabainisha kuwa Willy Gamba hakuwa amepanga kuwa akifika Lusaka nchini Zambia atakutana na Amanda, msichana anayefanya kazi katika upelelezi nchini humo. Pia, Willy Gamba anaonekana kuwa hakuwa amepanga kuwa ataingia katika penzi la Amanda wakati akiwa katika hatua za shughuli zake za kipelelezi. Vilevile, hakutarajia kuwa Amanda atachochea moyo wa kijasiri kwa kumtia moyo kuanza harakati za mapambano yake. Hivyo, jambo hilo lilitokea kwa sadfa. Katika kuipambanua sadfa hii, mwandishi anasimulia:

> …Wale wasichana nao waliwahi kumtupia jicho Willy, ingawaje kwa wasiwasi na kuendelea na kazi zao kana kwamba hakuna aliyeingia humo ndani… Alikuta wale wasichana bado wapo. Yule msichana aliyekuwa anashughulika na simu pamoja na teleksi alikuwa bado yu kazini, wakati yule msichana mwingine aliyekuwa akipiga taipu alikuwa amekaa juu ya meza huku ameshika mkoba wake huku akionesha kuwa amemaliza kazi. Walipomwona Willy anatokeza, yule msichana aliyekuwa amekaa kwenye meza aliteremka haraka haraka na kujiweka sawa. (uk. 32)

Masimulizi hayo kutoka katika riwaya teule yanathibitisha kuwa ni sadfa pekee ndiyo ilisababisha Willy Gamba akutane na kufahamiana na Amanda. Vilevile, inadhihirisha kuwa kuhitaji usafiri kwa Amanda ili arudi nyumbani kinakuwa ni kichocheo kikubwa cha kuunda mahusiano baina yake na Willy Gamba. Katika kuzidi kuthibitisha kuwa sadfa inatumika kama kitangulizi cha shughuli za kishushushu na kijasusi kwa mantiki ya kutiana moyo, mwandishi anaendelea kusimulia:

> "Mwambie mzee, mimi nimemaliza kazi; naomba anifanyie mpango wa usafiri kurudi nyumbani."

> Wakati yule msichana mwingine akizungumza na bosi wao, Willy ambaye sasa alikuwa amewasogelea karibu akiwaangalia kwa makini wale wasichana, alimtolea yule msichana aliyekuwa akiomba usafiri tabasamu la haiba kisha akamwambia, "Hamna haja ya kuomba usafiri. Kama hutajali nitakupa msaada mahali popote unapotaka kwenda" (kur. 38 na 39).

Nukuu hapo juu inaonesha mazungumzo kati ya Willy na Amanda. Kupitia mazungumzo yao wanajikuta wanaelekea kupata kinywaji katika baa mojawapo jijini Lusaka na kisha mazungumzo ya kimapenzi yakamea baina yao kama mwandishi anavyoelezea:

> "Kama mimi ningekuwapo hapa siku zote, amini nakwambia, ningepata tu muda." Alimjibu huku wakikaa kwenye meza moja kando ya bwawa lililotengenezwa hapo Ridgeway. Mtumishi alikuja akaagizwa vinywaji. Vinywaji vilipokuja walikunywa huku wakielezana mambo mbalimbali katika maisha yao ambayo yaliwafanya kushtukia ni saa sita na sasa walitakiwa waondoke" (uk. 41).

Katika kuonesha namna bahati nasibu ya makutano yao ilivyomea, mwandishi anazidi kusimulia kuonesha namna Amanda alivyojikuta tayari yupo katika mikono ya Willy Gamba kimapenzi. Huba hilo zito linathibitishwa katika mazungumzo ya faragha baina yao kama inavyodhihirika hapa chini:

> "Asante sana Willy. Umenifanya kuwa msichana wa furaha sana leo kwani, kwa mara ya kwanza maishani, nimepata mtu ambaye nimeweza kuzungumza nae na kunielewa. Tafadhali ukirudi toka Kinshasa, fanya juu chini unione. Mungu atakusaidia, najua utarudi salama. Kwa hiyo, tafadhali rudi hapa unione, eh Willy?" (uk. 41).

Licha ya Amanda kujua kuwa kazi anayoenda kuifanya Willy Gamba jijini Kinshasa ni kazi ngumu lakini bado anampa moyo kuwa atarudi salama. Hivyo, maneno ya Amanda yanazidisha ari ya Willy, naye haishi kuonesha kuwa endapo atarudi salama bila mashaka atapitia Lusaka kwa ajili ya 'kutia mbolea' penzi lake na Amanda. Hili linathibitika kama mwandishi anavyobainisha:

> "Mungu akipenda nikiwa salama, nitakuja usiwe na shaka." Willy alijibu huku wakiingia ndani ya gari huku akimvuta Amanda na kuanza kumpiga busu. "Tafadhali urudi!" alimnong'oneza (uk. 41).

Hivyo basi, tunaona namna sadfa ya kimapenzi ilivyoundwa na mwandishi kwa lengo maalumu la kutoa hamasa kwa kazi ngumu ya kishushushu na kijasusi ambayo ilikuwa inamkabili Willy Gamba. Mahusiano yaliyoibuka kati yake na Amanda imejidhihirisha kuwa yaliundwa kama chachu ya kumtia nguvu kwenda kuifanya kazi aliyokabidhiwa na kamati maalumu ya idara za kipelelezi za nchi zilizo katika mstari wa mbele wa ukombozi wa nchi za kusini mwa Afrika.

**2.2 Sadfa ya Kimapenzi Hurahisisha Operesheni ya Upelelezi**

Mwandishi kupitia masimulizi yake ameitumia mbinu ya sadfa ya kimapenzi ili aweze kuleta urahisi wa kufanikisha majukumu ya wahusika wake muda wote wa operesheni zao za kipelelezi. Kupitia wahusika wake Willy Gamba na Ntumba, mwandishi ameifinyanga sadfa husika kwa lengo tajwa. Ntumba ni binti anayefanya kazi katika kampuni ya ukodishaji wa magari inayoitwa *Societe de Transport de Kinshasa* maarufu kama S.T.K. Kampuni hiyo Willy Gamba anaitumia kukodi gari analolitumia katika harakati zote za mapambano dhidi ya majasusi yaliyo chini ya mwamvuli wa shirika la kijasusi la makaburu wa Afrika Kusini liitwalo BOSS.

Ukitazama kwa makini, Willy Gamba hakupanga kuwa akifika Kinshasa atakutana na Ntumba. Lakini makutano yao yanazalisha hisia za mapenzi na yanaleta tija kubwa kwa kazi ya ujasusi anayoifanya Willy Gamba. Ingawa Willy Gamba hakuwa amezama kabisa kwa Ntumba, lakini 'kujigonga' kwa Ntumba kwa kiasi kikubwa kunasaidia operesheni za wapelelezi wa nchi huru zilizo katika mapambano dhidi ya makaburu. Mwandishi anayafunua mahusiano ya Willy na Ntumba kama pindi Willy Gamba anapohitaji kukodi gari kwa ajili ya shughuli za kijasusi walizotarajia kuanza kuzifanya nchini Zaire. Katika kuthibitisha kuwa 'kujigonga' kimapenzi kwa Ntumba kunakuwa turufu kwa Willy Gamba, mwandishi anabainisha:

> "…Nimekuchagulia gari nzuri sana na mpya aina ya Mercedes Benz, ina redio *cassette* ndani yake, kwa hiyo naamini itakufaa sana, hasa kwa mfanyabiashara kama wewe. Na ukipata matatizo yeyote tafadhali nijulishe. Kadi yangu ya kazi hii hapa," alimpa kadi hiyo Willy akaiangalia. Ilikuwa na jina la msichana huyu ambaye aliitwa Ntumba Akanda. Vilevile kulikuwa na nambari za simu yake ya nyumbani pamoja na ya kazini.
> "Asante sana, Ntumba. Nikipata shida yeyote nitakujulisha."
> "Hata ukikosa mahali pa kulala, karibu nyumbani." Alitania huku akicheka.
> "Lo! Afadhali nikose nafasi ili nikaribishwe kwako." Willy naye alijibu kwa utani.
> "Asante sana, bibie. Tutaonana." (kur. 44-45)

Katika kurasa za mbele za riwaya hii, tunakuja kubaini namna Ntumba anavyomsaidia Willy Gamba kupata taarifa za gari lililotumiwa na majasusi. Taarifa hizo muhimu zinaanza kumsaidia kuanza kufahamu nyendo za maadui zake. Mwandishi analibainisha hili kupitia mazungumzo ya simu kati ya Willy Gamba na Amanda kama ifuatavyo:

> "Nakuomba unieleze kitu fulani, lakini kiwe siri unasemaje?"
> "Uliza tu. Toka juzi nimekwambia hata ukitaka kukaa nyumbani kwangu itakuwa siri yangu."
> "Jana mchana kuna gari lenu lilipatwa na ajali katika barabara ya *Poid Lourds*. Unaweza kuniambia nani alikuwa amelikodi?"

> "Gari hilo lilikuwa limekodiwa na kijana mmoja wa kizungu aitwaye Charles. Aliacha anuani yake na tulikuwa na nambari ya leseni yake ya kuendeshea. Kitu cha ajabu ni kwamba anwani aliyotuachia na leseni vyote ni vitu bandia. Kwa hiyo tunahisi hata jina lake ni la bandia vilevile. Je, una la zaidi?"
> "Sina zaidi. Asante sana." (kur.127-128).

Ntumba anaendelea kumpatia Willy Gamba habari muhimu kuhusu gari la majasusi Mulumba na Kasongo lililokuwa linawafuatilia. Pia, Ntumba anamsaidia Willy dhidi ya polisi waliokuwa wakipeleleza muuaji wa mwanadada Mwadi. Ntumba anawadanganya kuwa polisi alikuwa na Willy baada ya Willy Gamba kumsihi afanye hivyo. Mwandishi anasimulia hivi:

> "Mwanaume wewe, kila siku wewe una tatizo tu, tatizo langu mimi hutaki."
> "Hukuweza kunisaidia tatizo hili, tatizo lako nitalimaliza mara moja."
> "Haya sema tatizo lako, mimi niko tayari saa ishirini na nne kukusadia. Shauri yako wewe unayeniponda!"….
> "Sasa sikiliza kwa makini. Mimi nina tatizo kidogo na polisi. Mimi nimewaambia kuwa tulikuwa wote toka jana kiasi cha saa kumi na moja mpaka leo asubuhi. Nimewaeleza kwamba tulikuwa nyumbani kwako na kwamba hatukutoka mpaka asubuhi. Naomba wakikuuliza useme hivyo hivyo, tafadhali sana."
> "Umefanya nini, mwanamume wewe?"
> "Usitake kujua, tafadhali. Je, utafanya hivyo? Willy, alitaka kuhakikisha.
> "Siwezi kukuangusha, nitafanya hivyo. Je, jioni nitakuona?... (kur. 180-184).

Katika mahojiano kati ya Willy na polisi, tunaona Willy anawalaghai polisi kuwa hakuwa na Mwadi na hajui taarifa juu ya kifo chake. Willy anawapatia polisi maelezo yanayowiana na Ntumba na hivyo kuokoka kufuatiliwa na polisi kuhusu kifo cha Mwadi. Mwandishi anayaelezea wakati wa mahojiano ya Willy Gamba na polisi:

> "Unaweza kutueleza jana kuanzia kiasi cha saa kumi na moja jioni mpaka leo asubuhi ulikuwa wapi?"
> "Nilikuwa nimekaribishwa mahali"
> "Mahali gani?"
> "Kwa msichana mmoja."
> "Unaweza kututajia jina la huyo msichana?"
> Willy alisita kisha akasema. Anaitwa Ntumba Akanda."
> "Anakaa wapi?"
> "Anakaa huko Matonge, barabara ya Inzia, nyumba nambari 26 B."
> "Anafanya kazi?"
> "Ndiyo"

> "Wapi?"
> "S.T.K. uwanja wa ndege"
> "Una maana jioni yote ulikuwa huko na hukuondoka hata mara moja mpaka asubuhi"
> "Ndiyo."
> "Una lolote unaloweza kutuelezea juu ya mauaji ya Mwadi?"
> "Nimesikitika sana." (kur.183-185)

Baada ya mahojiano ya polisi na Willy, polisi wanamrudia Ntumba, naye anatoa maelezo yanayoshabihiana na maelezo aliyoyatoa Willy kama inavyojionesha hapo chini:

> Wale polisi walichukua simu na kupiga moja kwa moja S.T.K uwanja wa ndege. Waliomba waongee na Ntumba na walipompata walimwuliza kama alikuwa namfahamu Willy Chitalu. Baada ya mazungumzo marefu aliwathibitishia kuwa alikuwa na Willy tokea saa kumi na moja jioni mpaka asubuhi. Waliridhika wakaondoka (uk.185).

Kwa hiyo, hapa utaona namna sadfa ya kimapenzi ilivyotumiwa na mwandishi katika muktadha wa kumsaidia mhusika mkuu wa riwaya hii Willy Gamba ili aweze kupata urahisi wa kufanya kazi yake ya ujasusi. Urahisi huo kwa kiasi kikubwa ulisaidia operesheni za kijasusi za kina Willy Gamba zikamilike kwa mafanikio.

**2.3 Sadfa ya Kimapenzi Husaidia Uokozi na Huchochea Ulipizaji Kisasi**
Watunzi wa riwaya za kishushushu na kijasusi hutumia sadfa za namna mbalimbali katika kuwaokoa wahusika wao ambao ni wapelelezi dhidi ya hatari zinazowaandama. Sadfa ya kimapenzi ni namna mojawapo ambayo watunzi huitumia katika kuwaokoa wapelelezi hao. Makutano ya sadfa baina ya wahusika wa pande mbili huchipuza hisia za kimapenzi kati ya wahusika hao. Hisia ambazo huzaliwa katika hali ya sadfa huleta athari upande mmojawapo wa wahusika hao. Kwa kiasi kikubwa, mahusiano hayo huzalishwa na wahusika wawili wa makundi tofauti (wapelelezi na waovu). Upande mmoja hufaidika na sadfa hii ya kimapenzi, mara nyingi upande wa upelelezi hufaidika zaidi.

Katika *Kikosi cha Kisasi* tunaona namna ambavyo sadfa ya kimapenzi inamwokoa mhusika Willy Gamba dhidi ya mitego aliyotegewa na makaburu wanaomtafuta. Makutano ya sadfa baina yake na Mwadi (mhudumu wa hoteli) yanatumika kumwokoa dhidi ya wahalifu hao. Mahusiano ya wahusika hawa yanastawi na kufikia hatua ya kuanza kusaidiana na kustarehe pamoja kama mwandishi anavyobainisha:

> "Wakati ninatoka ulikuwa na shughuli nyingi usingeweza kuniona." Willy alijibu huku akianza kutambua kuwa msichana huyu alikuwa na kitu fulani ambacho kilikuwa kinaugusa moyo wake. Si kwamba Mwadi alikuwa msichana mzuri sana, la hasha!

> Alikuwa msichana mzuri wa kiasi tu, lakini kitu hiki alichokuwa nacho kilichokuwa kikigusa moyo wa Willy, kilimfanya Willy aamue kuwa karibu na msichana huyu ili aweze kukijua ni kitu gani hiki (kur. 69-70).

Katika kuthibitisha namna mwandishi alivyotumia mbinu ya sadfa ya kimapenzi kwa jukumu la uokozi na uchochezi wa kisasi, anabainisha jinsi ambavyo Mwadi anamwokoa Willy Gamba dhidi ya Muteba na watu wake kwa kutowapa jina lake kama mgeni aliyefika hotelini hapo:

> Mwadi, ambaye mara moja mawazo yake yale yalikwenda kwa kijana ambaye alikuwa amewasili mchana ule, alisita kisha akasema, sawa Kabeya. Nitashughulikia … Afadhali mimi nipate matatizo kuliko yule kijana, Mwandi alijisemea (uk. 62).

Makutano ya wahusika hawa wawili yanazidi kushamiri zaidi kwa kuzalisha mahusiano ya kimapenzi. Mapenzi baina ya Willy na Mwadi yanamkutanisha Willy na mhusika mwingine muhimu (Tete) ambaye anazidi kunogesha na kuchangamsha masimulizi katika riwaya hii. Kufahamiana baina ya wahusika hawa ni kwa sadfa tu, kwani makutano yao hayakupangwa. Walikutana wakati Tete anamtafuta mpenzi wake (Muteba). Makutano ya Willy na Tete yanazalisha hisia nyingine nzito za kimapenzi baina yao kama mwandishi anavyosimulia:

> Kisha yule msichana alimgeukia Willy, macho yao yakakutana. Macho ya huyo msichana yalikuwa malegevu, lakini yenye nguvu fulani ambazo zilimwingia hasa Willy.
> "Mbote!" Willy alisalimiwa.
> Willy alitabasamu na baada ya kusita kidogo alijibu, "Mbote!"
> Mara moja yule msichana alihisi kuwa huyo kijana aliyekuwa na Mwadi si mwenyeji wa Kinshasa wala Zaire. Msichana huyo alivutiwa sana na kijana huyo aliyekuwa na Mwadi naye akakata shauri kuvuta kiti, akakaa. (kur. 102-103)

Aidha, mazungumzo ya awali baina ya Willy, Mwadi na Tete yanampa Willy wasaa wa kufahamiana na Tete na kujua mahali anapofanya kazi. Anapata nafasi ya kukaribishwa katika ofisi yake anayofanyia kazi jambo linalokuwa na faida zaidi kwa upande wa Kikosi cha Kisasi:

> "Itakuwa vizuri sana. Kampuni yetu ni kampuni kubwa na inayojulikana sana. Hata imeweza kuwa wakala wa makampuni makubwa ya Afrika Kusini nchini Zaire. Kwa mfano, miezi miwili iliyopita tuliweka saini mkataba kwa niaba ya Serikali ya Zaire na; mkataba ambao ulikuwa kati ya Serikali na kampuni moja ya Afrika Kusini iitwayo *Grindrod Cots Stevedoring* ya mjini *East London* wa kusafirisha tani 125,000 za shaba ziendazo Japan kwa kupitia kwao. Hii itakuonyesha jinsi kampuni yetu ilivyo maarufu. Mimi naamini tunaweza kuwa na uelewano mzuri zaidi kati yetu na makampuni ya

> Zambia kuliko nchi nyingine yoyote." Tete alisisitiza (kur.104 - 105).

Kusikia maneno hayo moyo wa Willy ulipiga harakaharaka maana maelezo hayo yalikubaliana sana na maelezo aliyopewa na Robert juu ya uhusiano wa Zaire na Afrika Kusini kibiashara. Vilevile, alikumbuka wasiwasi wa Robert (shushushu mwenzie) kuwa makampuni yanayoshuhghulikia masilahi ya wafanyabiashara wa Afrika Kusini, yanaweza kutumiwa kiujasusi na nchi hiyo ambayo iko mstari wa mbele katika kupinga maendeleo ya nchi huru na zile ambazo bado zinapigania uhuru. Kimsingi, taarifa hizi zimedhihirika kupatikana kwa sadfa tu kupitia mahusiano ya kimapenzi kati ya wahusika waliojengwa na mwandishi.

Kitendo cha Mwadi kumwokoa Willy dhidi ya wahalifu kinamsababishia kifo cha kinyama. Mwadi anauawa kinyama na Kabeya kutokana na kukataa kumwambia chochote kuhusiana na Willy Gamba. Sadfa inazidi kudhihirika kutokana na nafasi ya mapenzi yaliyokuwapo baina yao, Willy anapata taarifa kuhusiana na wauaji hao kutoka kwa Tete na anakusudia kulipiza kisasi huku akikamilisha shughuli iliyompeleka Kinshasa:

> "Mama yangu mzazi!" Willy alilalamika kwa hasira. Mwadi alikuwa amekatwa kwa kisu na kulazwa kitandani matumbo yote nje! Yalikuwa mauaji ya kishenzi ambayo Willy alikuwa hajawahi kuyaona. Haraka haraka Willy alichukua shuka akaifunika maiti ile, akaangalia huku na huko, lakini hamkuwa na kitu chochote cha maana.
>
> Kwa uchungu akamsalia Mwadi kwa sauti, "Mungu mmoja, mpenzi wangu Mwadi, watu waliokufanya hivi, nitakulipizia kisasi kwa mkono wangu. Maana umekufa kwa ajili yangu. Nitakukumbuka daima." (uk.144).

Kitendo cha Willy kulipiza kisasi dhidi ya Mwadi, kinazalisha sadfa nyingine yenye mwegamo wa kimapenzi baina yake na Tete. Mahusiano hayo yanajenga mwelekeo mpya wa masimulizi ya riwaya. Willy anafahamishwa mambo ya msingi zaidi na Tete kuhusiana na shughuli zote za ofisi yao na namna ofisi yao ilivyojengwa ikitokea dharura:

> "Kwanza nataka kutoa shukrani zangu kwa kumlipizia kisasi rafiki yangu Mwadi."
>
> "Umejuaje kama nililipiza kisasi?"
>
> "Si uliniambia kuwa ungelipiza kisasi, kisha nikapata habari toka kwa Muteba kuwa Kabeya ameuawa. Basi sikuwa na shaka kuwa umelipiza kisasi"
>
> "Muteba alikueleza saa ngapi?"
>
> "Alikuja nyumbani kwangu kiasi cha saa kumi alfajiri" Kwanza tuache hayo. Tafadhali Willy, nataka unieleze bila kunificha chochote, wewe ni nani na uko hapa Kinshasa kwa ajili gani, halafu nitakueleza mambo ambayo ninaamini yatakuwa na manufaa

> kwako. Mpaka sasa hivi ninauza maisha yangu kwa ajili yako, tafadhali usinifiche"
> "Kwa nini ujitolee kuuza maisha yako kwa ajili yangu?"
> "Kwa sababu ileile ambayo ilimfanya Mwadi auze maisha yake kwa ajili yako. Mwadi alikuwa rafiki yangu mpenzi. Kwa hiyo, niko tayari kuendeleza chochote alichoacha bila ya kukimaliza" (kur. 187-188).

Hivyo basi, kupitia riwaya ya *Kikosi cha Kisasi* inathibitika kuwa mafanikio ya ukamilishaji wa shughuli za kijasusi na kishushushu hutegemea msaada toka katika mazingira ambayo matukio hayo yamefanyika. Mtunzi ametumia sadfa ya kimapenzi kutufahamisha matukio mengi ya nyuma kwa haraka zaidi. Sadfa hizi za kimapenzi zimetumika zaidi katika kuwafahamisha wapelelezi matukio na kuwakutanisha na wahalifu. Vilevile, zimetumika kuwanusuru katika mikono ya wahalifu hao.

### 2.4 Sadfa ya Kimapenzi Husaidia Uvumbuzi wa Taarifa Muhimu

Sadfa ya kimapenzi inadhihirika katika usaidiaji wa uvumbuzi wa taarifa muhimu za kijasusi na kuchagiza kukamilika kwa matukio ya kijasusi katika riwaya za kipelelezi. Mtunzi amemtumia mhusika (Willy Gamba) katika kuonesha namna anavyosaidiwa na sadfa hii ya kimapenzi kupata kujua yaliyojificha nyuma ya pazia kuhusiana na matukio ya mauaji.

Sadfa inawakutanisha Willy Gamba na Tete ambaye anakuwa msaada mkubwa kwa wapelelezi wa Kikosi cha Kisasi katika kukamilisha misheni yao ya kijasusi. Makutano yao yanazalisha hisia za kimapenzi baina yao, kupitia hisia hizo kunapatikana kwa taarifa za msingi kuhusiana na wauaji wa wapigania uhuru. Tunaona namna ambavyo wahusika hawa walivyokutanishwa Mwadi kama mwandishi anavyobainisha:

> Bila ya kuonyesha dukuduku lake Willy alisema, "Ni bahati ilioje kukutana na wewe, na inabidi nimshukuru Mwadi kunitambulisha kwako. Hivyo kampuni yenu ni ya Kizaire au ni watu kutoka nje?"
> "Hiyo kampuni inaongozwa na Wabelgiji. Lakini wamekuwa hapa kwa muda mrefu sana na wameweza kufanya biashara karibu na nchi zote za Afrika"
> "Vizuri basi, nitafika ofisini kwenu kesho. Ofisi zenu ziko wapi?"
> Tete alifungua kimfuko chake kidogo akatoa kadi yake ya biashara na kumpa Willy (kur. 104-105).

Makutano ya wahusika hawa yanaleta faida upande wa Willy Gamba kwa kukaribishwa katika ofisi ya *Agence Sozidime* ili afanye mazungumzo na Afisa biashara wa kampuni hiyo. Mipango yote hiyo inaratibiwa na Tete kabla ya Willy Gamba kufika. Mwandishi anathibitisha hili kwa kusimulia:

> Ofisi za *Agence Sozidime* zilikuwa ziko sehemu ya Gombe, mtaa wa *Avioteurs*, karibu na jumba la sinema liitwalo *Cine Rae*. Habari

> zote hizo zilikuwa kwenye kadi ambayo Tete alikuwa amempa Willy, hivyo haikuwa vigumu kwa Willy kuipata ofisi hiyo. Willy aliipata ofisi hiyo karibu na *Cine Rae*, kama ilivyokuwa imeelezwa kwenye kadi. Ofisi yenyewe ilikuwa ndani ya nyumba moja ndogo ambayo ungefikiri ni nyumba ya kuishi mtu binafsi. Ilikuwa imezungukwa na michongoma mirefu ambayo ilikuwa inaimeza nyumba na mbele kulikuwa na lango kubwa… (kur.134-134).

Makutano yao ya awali yanazalisha manufaa zaidi kwa Willy na Kikosi cha Kisasi kwa kufahamu kwa undani baadhi ya mambo yaliyojificha kupitia makampuni ya kigeni. Mazungumzo kati ya Willy Gamba na Max (Meneja Biashara wa *Sozidime*) yanamshtua Willy Gamba kwa kuhusishwa na masuala ya kisiasa. Mshtuko huo unamjengea shauku ya kufanya upelelezi zaidi kuhusiana na ofisi hiyo (kur. 137-138).

Baada ya mazungumzo ya Willy Gamba na Max, Willy anakutana na mauaji ya mpenzi wake (Mwadi). Hata hivyo, Tete anamfahamisha watu wanaohusika na mauaji ya Mwadi kama mwandishi anavyobainisha:

> "Kama kweli alikuwa rafiki yako, mimi nataka kukulipizia kisasi. Sasa lazima unisaidie. Kuna mtu amekuuliza habari za Mwadi leo?" Willy aliuliza baada ya kuona Tete analainika.
> Tete alianza kufikiria jinsi mpenzi wake Muteba na rafiki yake Kabeya walivyokuja saa kumi ile baada ya kutoka kazini na kumwuliza juu ya Willy na Mwadi. Sasa alishangaa kusikia Mwadi ameuawa" (uk.146).

Baada ya kufahamishwa kuhusiana na wauaji hao, pia alielezwa kuhusiana na shughuli zao hapo Kinshasa. Anaelezwa pia namna anavyotafutwa na wahalifu hao. Masimulizi yananogeshwa kwa namna wahusika hawa wanavyoanza kutafutana. Sadfa ya mapenzi inamsaidia zaidi Willy Gamba kwa kufahamu wanapoishi wahalifu hao:

> Willy alianza kuona mwanga mkubwa sana sasa. Kumbe *Sozidime* ilikuwa na uhusiano na hayo magereji ya majambazi. Jambo hilo lilimpa dukuduku kubwa sana moyoni (uk.148).

Baada ya kulipiza kisasi kwa Kabeya, Willy anapata taarifa muhimu zaidi kuhusiana na majasusi wa Afrika Kusini kama mwandishi anavyobainisha hapo chini:

> "Kabeya, sema WP ni chama gani?" Kabeya aliinua macho na kumwangalia Willy huku sauti ikiwa inafifia anasema, "*White…po…po…power*." Halafu akakata roho. Willy aliondoka ndani ya nyumba hiyo. Akiwa anatembea kwa haraka, aliingia ndani ya gari lake kuelekea nyumbani kwa Robert (uk.154).

Halikadhalika, Tete anamueleza Willy taarifa muhimu kuhusu Mkurugenzi wa *Sozidime* anayeitwa Fernand Barbier ambaye anadai kuwa ni Mzungu lakini kumbe ni kaburu. Pia, Mkurugenzi wa *Garage du Piple*, yaani Pierre Simonard

naye si Mbelgiji bali ni kaburu pamoja na Jean Vergeance. Vilevile, Tete anamsaidia Willy kufahamu kuwa kumbe Maximilian bosi wa *Sozidime* ambaye aliongea naye si Mfaransa bali ni jasusi wa BOSS. Habari zote hizo Tete alizipata kutoka kwa mpenziwe Muteba ambaye alishawahi kukodishwa kama askari wa majeshi ya Tshombe huko jimbo la Shaba (kur. 188-189).

Tete pia anamweleza Willy juu ya jengo la Sozidime na chumba cha siri kinachotokea mbali na jengo hilo ambalo kinaweza kutumiwa kujificha au kutoroka. Chumba hicho Tete alifanikiwa kuoneshwa na kuingia pamoja na Max. Alimweleza Willy kuwa handaki lilikokuwamo katika chumba hicho lilikuwa linatokea nyuma ya jengo la refu la '*Gallaries Presidentielles*'. Max alimweleza yote hayo Tete kwa kuwa alikuwa anamtamani kimapenzi (kur. 190-191).

Vilevile, Tete anampa taarifa Willy kuwa wameshagundua kuwa yeye ni mpepelezi maarufu Willy Gamba na si Willy Chitalu kama anavyojinasibu. Yote haya yanamsaidia Willy kufahamu kuwa Maxmilian ni jasusi wa Shirika la Ujasusi la Ufaransa, SCEPE na anang'amua jinsi ambavyo CCEPE, BOSS na CIA zinavyofanya kazi kwa kushirikiana ndani ya bara la Afrika (uk.192).

Kwa kiasi kikubwa Tete anakuwa msaada wa operesheni nzima ya kipelelezi. Kupitia utumiaji wa mbinu ya sadfa ya kimapenzi, mwandishi anatuonesha kuwa mapenzi ya Tete kwa Willy yanamfanya ajitoe mhanga kwa kuendesha gari wakati wote wa mapambano hadi wanafanikiwa kwa pamoja na kuleta ushindi kwa kamati maalumu ya kuleta ukombozi wa nchi huru za Kiafrika (kur. 205-226). Ushindi huo kwa Kikosi cha Kisasi ukawa ni kikomo cha masimulizi ya riwaya.

## 3.0 Hitimisho

Makala haya yamefafanua namna sadfa ya kimapenzi inavyotumika katika riwaya (hususani za kipelelezi) kwa minajili ya ujenzi wa matukio ya kishushushu na kijasusi. Katika kulifafanua suala hili, tumeona sadfa ya kimapenzi katika riwaya za kipelelezi ilivyotumika na mwandishi katika miktadha ya kutiana moyo ya kuelekea katika ufanikishwaji wa operesheni za kishushushu na kijasusi, kuleta urahisi wa ufanikishaji wa shughuli za kishushushu na kijasusi, kusaidia uokozi na uchocheaji kisasi pamoja na sadfa ya kimapenzi kwa ajili ya uvumbuzi wa taarifa muhimu za kijasusi pamoja na ukamilishaji wa operesheni za kijasusi. Ujitokezaji wa sadfa ya kimapenzi katika riwaya umefanyika kupitia riwaya ya *Kikosi cha Kisasi*. Suala la sadfa ya kimapenzi lilijitokeza kupitia mahusiano ya kimapenzi baina ya mhusika Willy Gamba (mwanamume) pamoja na mabinti Amanda, Ntumba, Mwadi na Tete.

## Marejeleo

Bwimbo, P. D. M. (2015). *Mlinzi Mkuu wa Mwalimu Nyerere*, Dar es Salaam: Mkuki na Nyota.

Chahali, E. (2016). *Afisa Usalama wa Taifa (Shushushu): Ni Mtu wa Aina Gani? Na Anafanya nini?* Aberdeen: delPhil Consultancy.

Dannenberg, H. (2008). *Coincidence and Couterfactuality: Plotting, Time and Space in Narrative Fiction*. Nebraska: University of Nebraska Press. Kimesomwa kutoka http://www.jstor.org/stable/j.cttldgn486.

Kageuka, F. (2016). *Mateka Mpakani*. Dar es salaam: Upendo Frowin Publishers.

Kyando, L. (2012). "Majina ya Sadfa katika Kusadikika na Kichwamaji," katika *Mulika*, Juz. 31. Dar es Salaam: Taasisi ya Taaluma za Kiswahili. 37-51.

Madumula, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publishers Ltd.

Musiba, A. (2018). *Kikosi cha Kisasi*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publisher Limited.

Snowden, E. (2019). *Permanent Record*. New York: Metropolitan Books & Henry Colt.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishing Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: *Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.